


UWIANO WA SHERIA ZA MBEGU ZA AFRIKA KUPITIA KANDA YA SADC NA COMESA



Uwiano wa sheria za mbegu inamaanisha kuwa nchi zote katika kanda zitatumia mifumo sawa ya kutolea aina ya mbegu, taratibu sawa za kuthibitisha na kufanya majaribio ya mbegu na kutumia mbinu sawa za karantini na usafi kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu. Kutakuwa na *Orodha ya Mbegu ya Kanda* au *Katalogi ya Mbegu ya Kanda* moja inayotoa maelezo ya aina za mbegu zilizoidhinishwa na mamlaka kuu ya kutoa maamuzi kwenye kanda. Hii inamaanisha kuwa, iwapo aina ya mbegu itaidhishwa na kuwekwa kwenye Orodha ya Mbegu ya Kanda, aina ya mbegu itakayotolewa na kujaribiwa kwa misimu miwili tu katika nchi moja inaweza kuzalishwa na kuuzwa pia katika nchi zingine zote katika kanda hiyo.

Uwiano wa sheria za mbegu barani Afrika unasimamiwa na jumuiya za kiuchumi katika kanda (RECs). Mfumo wa uwiano wa sheria za mbegu ndani ya Jumuiya ya Maendeleo ya Afrika za Kusini mwa Afrika (SADC) inatumika katika nchi wanachama 15, wakati usimamizi wa uwiano wa sheria za mbegu ndani ya Soko la Pamoja la Afrika ya Mashariki na Kusini (COMESA) inatumika katika nchi wanachama 19. Nchi binafsi zinalazimika kurekebisha sheria zake za mbegu ili kuzingatia mchakato wa uwiano kikanda. Hii inamaanisha kuwa mfumo wa usimamizi wa mbegu kikanda utakuwa na mamlaka zaidi kuliko serikali ya nchi kuhusu aina mbalimbali za mbegu zinazotolewa kikanda.

Uwiano unalenga kuongeza biashara ya mbegu kikanda na majukumu ya makampuni binafsi kwenye uzalishaji na usambazaji wa mbegu katika nchi kadhaa. Hii itatengeneza soko kubwa la mbegu kwa makampuni haya.

